SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

www.swahiliweb.net

Archive: Pat Caplan

Document: Interview with Mwavura binti Silima

File reference: SW/PC/13016

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Interview with Mwavura binti Silima 1985, transcribed by Joseph Bwaithondi Jan. 2011**

*Mwavura was an elderly neighbour living on her own, although children, grandchildren and several great-grandchildren lived nearby.*

*NB: PC = Pat Caplan, MS =Mwavura binti Silima. Other people who appear in this conversation are a three other men and a woman.*

MS: We mama kwako wapi?

PC: Ulaya (Uingereza)

MS: Ah! Uingereza.

PC: Mmh!

MS: Umekuja na ndege?

PC: Nimekuja na ndege mpaka Dar es salaam. Nimepanda ndege kubwa mpaka Dar es salaam halafu nikapanda ndege ndogo mpaka Kilindoni.

MS: Kufika Kilindoni ndio ukaingia garini?

PC: Ndio, umefika Kilindoni?

MS: Nimefika. Kilindoni nikujua

PC: Dar es Salaam?

MS: Sikujui mama.

PC: Unguja?

MS: Sikujui Unguja wala Dar es salaam. Wakati wetu tulikuwa tukitembea kwa miguu ndio maana nakujua Kilindoni. Mpaka ilipokuja gari mie tena sikuwahi kwenda.

PC: Unatembea kwa miguu mpaka Kilindoni?.

MS: Mpaka Kilindoni.

PC: Kwani kufuata nini?

MS: Kutembea tu kule kufuata wazee wangu walikuwa wakiishi kule.

MS: Zama zetu hatukuwa na gari. Maisha yenu ndio upande gari mpaka Kirongwe halafu upande nyingine mpaka Kilindoni

Stranger: Jirani amekwenda wapi?

MS: amekwenda kwake.

 ©Pat Caplan 2013

MS: Mbona mmerudi kulikoni?

Stranger: Nimezuiwa nyumbani kwamba havina kamba ( wale ng'ombe wadogo) hawana kamba. Ndio nimerudi nipate kamba hivi kidogo.

MS: Yeye mwenyewe yuko wapi?

Stranger: Mie sikumuona walahi

Stranger: Mama huyu ng'ombe hachinjwi?

PC: Sijuhi

Stranger: Au wewe hauli?

PC: Sili.

Stranger: Hata huyu.

MS: Aha! Basi ninunulie.

Stranger: Sina chenji ningekununulia. Mama ngoja niame nije kukupa ngoma za kizamani.

PC: Ngoma gani?

Stranger: Vanga

MS: Pesa umechukua na ulisema ungetuletea sinema huku. Na picha pia.

PC: Mbona zilishaletwa toka mwaka wa juzi hakuziona?

MS: kuziona nimeshaziona. Unamtaka mwanamke huyu?.

MS: Wanahama watu mpunga umekauka

PC: Ehe!ndio nimesikia

MS: Jua limekuwa kali moja kwa moja, hata kagunia kamoja hupati.Sijuhu zinapotoka chakula

PC: Wapi

MS: Huko mijini sijuhi mvua inanyesha huko bara

PC: Sijuhi. Wengi naona hafadhali kalima wapi?

MS: Nani?

PC: Wewe

MS: Huko Kapongo. Unapajua?

 ©Pat Caplan 2013

PC: Napaju ndio. Nilikwenda mwaka juzi

MS: Ndio huko alipolima baba yako. Sasa unakaa jikoni unapika wali unakula.

PC: Ndio, siku nyingine napika, nanunua au siku nyingine napewa.

MS: Mbona hakuja na baba?

PC: Anafanya kazi anashughulika na shughuli zake

MS: Kazi gani?

PC: Kazi yake ni ya kusomesha.

MS: Na watoto wako wanasoma?

PC: Wanasoma.

MS: binti yako akisha maliza kusoma anolewa ?

PC: Bado.

MS: Hakuvunja ungo?

PC: Mtoto wangu?

MS: Ndio

PC: Bado sana

MS: Umeonana na Naimu

PC: Yupi?

MS: Wa  Hamadi Mwatanda.

PC: Nilimuona. Nilifikiri mtu mwingi.

MS: Ulimjuona.

PC: Alikuja jana.

MS: Watoto wake wale waliolewa na kuachwa

PC: Nasikia

MS: Ka kwambia mwenyewe?

PC: Kaniambia mwenyewe na huyu mmoja  kaniambia.Nimsaidie kaachwa.Sasa atafanyaje?

MS: Hapana cha kufanya. Yeye akae tu. Manake alipata mtoto akiwa nyumbani kasha akaolewa  huko kusini. Akarudi tena nyumbani akapata


©Pat Caplan 2013

mtoto yeye mwenyewe. Dada yake naye kaacha vilevile. Yeye alipata watoto wawili ,

PC: Pacha?

MS: mmoja kafa moja yupo mzima

PC: Nauliza  watoto wawili pacha?

MS: Ndio. Basi mmoja kaondoka na mmoja yupo. Aliolewa na mwanaume sasa kaachwa.

PC: Wewe umewahi kuachwa mama?

MS: Mie.

PC: Ndio

MS: Ndio nilishawahi kuachwa.

PC: Na mume wa kwanza?

MS: Mie??

PC: Nakuuliza hivi umewahi kuolewa mara ngapi?

MS: Mara hizi

PC: Mara tano!

PC: Alhaula

MS: Kicheko

PC: Ebu niambie mume wa kwanza ni nani?

MS: Mume wa kwanza ni Peter Kama uliwahi kusikia wakiita angua angua ndio huyo  mjukuu wangu

PC: Je ulizaa naye?

MS: Huyu mtoto akiitwa Angua ni mtoto wa mwanangu wa kwanza kutoka katika ndoa ya kwanza. Mtoto wangu wa kwanza sikumposa. Yeye alikufa.

PC: Alikuwa kiume au kike

MS: Baba Yule alikuwa wa kiume

MS: Nikaja kuolewa jimbo nikaja kuzaa nae watoto wanne wa kike mmoja na wakiume watatu  na wamekufa wawili na wamebaki wawili wa kike mmoja na wakiume. Wanamme wawili

MS: Tena nikaja kuolewa tena  na Mwalimu Ali  nikazaa mtoto mmoja

 ©Pat Caplan 2013

PC: Huyu wa jimbo kakuacha au

MS: Kafa

PC: SAbabu gani ukaachwa?

MS: Tulichokana tu basi nikaachwa. Sasa baba utakae mpaka makelele aha wapi. Mkichokana basi

PC: Mimi sitaki kuachwa sitaki kabisa.

Mtu1: bibi salama

MS: Salama tu

MS: Hivi mama wazee ungalinao? Sasa mama ukitoka hapa unaenda kuona wazee wako?

PC: Wazee??

MS: Wazazi.

PC: Mama alishakufa ila baba yu hai.

MS: Baba yu hai?

PC: Ndio.

MS: Ameotena?

PC: Ameoa tena

MS:  Wewe peke yako au na dada zako?

PC: Ndugu zangu wawili

MS: Bado wapo nyumbani?

PC: Wameshaolewa zamani gani Mmoja amezaa watoto saba na wapo wote na huyu mwingine mdogo amezaa watoto watatu

MS: Ameshaoza

PC: Bado ngali wadogo.

MS: Utakapoondoka huku utaenda kumuona baba yako.

PC: Ndio nitakwenda kumuona.

PC: Nimpigi picha mjukuu wako huyu?

MS: Nimpige picha?


©Pat Caplan 2013

PC: Anasema hivi nimpige picha mjukuu wako?

MS: Sijui mama ye

PC: Si nitampatia mamaye halafu sura ya mwanae? Mgeuze ili nipate sura yake. Ngoja nimpige halafu nikija siku nyingine nitakupiga na wewe ukiwa umevaa nguo  nzuri.

MS: Sina nguo nzuri.

PC: Kwani watoto hakununuli nguo ?

MS: Wala haninunuli.

MS: Sasa wewe mama ng'ombe huli?

PC: Sili

MS: Kwa nini?

PC: Sitaki tu.

MS: Sasa leo watachinja minyama mingi tu

PC: Wewe ng'ombe hauli?

MS: Sili.

PC: Sababu gani?

MS: Tangu niwe mtoto sili tu

MS: Sasa mama mume umemuacha mwenyewe? Si ungekuja nae akatembee?

PC: Ana kazi zake

MS: yaani miezi mitatu unamuacha mume mwenyewe

PC: Kwani haifai

MS: aha!

Mwanamke: Salama.

PC: Salama

Mwanamke: Habari za mume na watoto?

PC: Salama kabisa. Na wewe mume hajambo

Mwamamke:  hajambo, siku ile tulikuona njiani kwenye gari tukakupungia ili utupatie msaada wa kutubebea mtoto manake tulikuwa tumechoka kumbeba sana.

 ©Pat Caplan 2013

PC: Gari limejaa hakukua na nafasi. Hupo wapi siku hizi

Mwanamke: Nipo hapa

MS: Ameamia shamba huyu

Mwanamke: Unanifahamu lakini

PC: Nakutambua ila jina limenitoka kidogo.

Mwanamke : Nilikuwa nakaa wapi?

MS: Haujaja wakati ule

MWanamke: hataa. Wakati ule nilishaolewa  mpaka na kuzaa.

PC: Nimesahau. Kwa ulikuwa ukikaa wapi?

Mwanamke: Kwa mzee Mchande

PC: Kwa Mchande.

MS: Kwa mchande huyo.

Mwanamke: Mie ni binti yake.

PC: Jina lipi?

Mwanamke: Chapa

PC: Chapa. Umeshapata watoto wengine?

Mwanamke: Nilipata watoto wanne na nimeshaposa na nimeshapata wajukuu.

MS: Ameshapata mjukuu.

Mwanamke: Nilipata wanaume na wakike  na nilishaposa wa kike na wakiume na harusi , wewe vipi umeshaolewa?

PC: Nimeolewa

Mwanamke: Umepata watoto?

PC: Wawili

Mwanamke: Wakike na kiume?

PC: Mojamoja

Mwanamke: wapo wapi?

PC: Wapo nyumbani wanasoma shule

Mwanamke: Bwana yupo wapi?


©Pat Caplan 2013

PC: Yupo nyumbani vilevile

Mwanamke: Sasa wewe huku naye  kule?

PC: Yupo nyumbani ana kazi yake

Mwanamke: Jana walikuja jamaa zako

PC: Ni jamaa tu.

Mwanamke: Walikuja kukutazama

PC: Walikuja kwa shughuli zao tu

Mwanamke: Sasa mama nipige picha

PC: Kaa

Mwanake : si mpaka nivae.

PC: Hivyo hivyo utapendeza wewe utakaa tu.

Mwanamke: Yaani tayari

PC: Mwanao huyu.

MS: Ndio.

Mtu3: Salama

PC: Salama.

MS: Naona anaumwa tumbo huyu. Hivi hii nini

PC: Mwavuli. Tunategemea mvua leo. Haya mie nakwenda zangu ofisini.

MS: Haya kwa herini


©Pat Caplan 2013